

# KUZIKWA



Baba wa Mbinguni aliyebarikiwa, pamoja na—na Uwepo wa Roho Mtakatifu ulio hapa tayari, tunalikaribia Neno Lako Takatifu. Na ingawa ni kwa sauti mbaya ninayojaribu kuzuia, na kuyatamka maneno polepole na thabiti niwezavyo, ninaomba mwongozo Wako wa Kiungu na upako wa Roho Mtakatifu utende kazi miongoni mwetu usiku wa leo. Na jalia Yeye Aliye kila mahali, jalia alichukue Neno la Mungu na kulipatia kila moyo, kadiri tu tunavyohitaji. Jalia atulishe usiku wa leo, juu ya mambo mazuri ya Mungu.

<sup>2</sup> Na usiku wa leo, tunapozungumza juu ya Neno, mioyo yetu na iwe maili nyingi ndani ya Kalvari, ambapo Yesu alilipia gharama ile itoshelazayo kwa yote yaliyohitajika na hukumu kuu za Mungu, kutoka bustani ya Edeni. Na leo hii na tutambue ya kwamba tunahesabiwa haki bure kwa kufufuka Kwake, na kwa kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka.

<sup>3</sup> Na usiku wa leo sisi sio wa ulimwenguni tena, kwa kuwa tumenunuliwa kwa bei ya Damu ya thamani ya Mwana wa Mungu. Basi jalia sisi, kwa mioyo yenye shukrani, tukugeukie Wewe usiku wa leo, kwa akili zote na nguvu zote, na tulizo nazo ndani yetu, na kukutumikia Wewe kwa moyo safi, usioghoshiwa.

<sup>4</sup> Jalia usiku wa leo, Baba, kukiwako na wengine hapa wasiokujua Wewe, katika msamaha wa dhambi zao, jalia usiku huu waje msalabani kwa unyenyekevu, na hapo waungame dhambi zao kwa Mungu aliye wa haki, kusamehe. Na jalia huu uwe usiku mzuri sana kwetu sote. Tunaomba katika Jina la Mwanao, Bwana Yesu. Amina.

<sup>5</sup> Sasa tunatambua kwamba hakuna mtu, duniani, ambaye anaweza vya kutosha kulichukua Neno la Mungu na kulifunua, kwa maana Neno limeandikwa kwa uvuvio. Roho Mtakatifu ndiye Mwandishi wa Neno.

<sup>6</sup> Na wakati mtu alipotafutwa, Mbinguni, kukitwaa kile Kitabu na kuifungua ile Mihuri, hapakuonekana mtu Mbinguni, wala duniani, wala chini ya nchi, ambaye alistahili kuifungua ile Mihuri, ama hata kukitazama kile Kitabu. Basi palikuwapo na Mwana-Kondoo Pale aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, Naye akaja akakitwaa kile Kitabu katika mkono wake Yeye aliyeketi juu ya kile Kiti cha Enzi, na kuifungua ile Mihuri na kulifungua Neno.

<sup>7</sup> Nasi usiku wa leo tunamwamini na kumtumaini Yeye, ya kwamba atatufungulia Neno, na sasa ninaposoma katika mlango wa pili wa Matendo.

<sup>8</sup> Nilivyotangaza, usiku wa kwanza ulikuwa *Kuja Kwa Pili*, na...kwa Bwana Yesu, kwamba ni Jumatano. Na Alhamisi

usiku ilikuwa juu ya *Sadaka Itoshelezayo Kwa Yote*. Na Ijumaa usiku ilikuwa ni *Upatanisho Utoshelezao Kwa Yote; Ukamilifu*. Mliupata jana usiku? *Ukamilifu*, jinsi tunavyoweza kuwa bila hatia na wakamilifu kabisa mbele za Mungu! Basi usiku wa leo ni *Kuzikwa*. Na kesho, *Ufufuo*. Kama vile tu siku zinavyofuatana.

<sup>9</sup> Sasa nimechagua usiku wa leo, kwa somo langu la Maandiko, kutoka katika Kitabu cha Matendo, mlango wa pili na vifungu vya 25, 26, na 27, vyote pamoja. Na inasoma hivi, Petro akizungumza.

Daudi, *maana Daudi* alizungumza *habari zake, Nalimwona Bwana mbele ya uso wangu siku zote, kwa kuwa yuko mkono wangu wa kuume, nisitikisike:*

*Kwa hiyo moyo wangu ukapendezewa, ulimi wangu ukafurahi; tena mwili wangu nao utakaa katika matumaini:*

*Kwa maana hutaiacha nafsi yangu katika kuzimu, wala hutamtoa Mtakatifu wako aone uharibifu.*

<sup>10</sup> Ni somo zuri jinsi gani la usiku huu, la kupata muktadha Wake akiwa kaburini.

<sup>11</sup> Jambo la kwanza tunalotaka kuangalia . . . kuuvutia usikivu wenu, ni kule kutoweza kukosea kwa Neno la Mungu. Mungu hulitimiza Neno Lake, kikamilifu. Na usiku wa leo tunataka kuyafungia mawazo yetu juu ya jambo hilo, ya kwamba Mungu hulitimiza Neno Lake. Tunaweza kuwa na uhakika wa jambo lolote ambalo Mungu amesema katika Neno Lake, kwamba ni Kweli. Wala imani haitulii juu ya mawazo ya mwanadamu yanayobadilika-badilika au theolojia au mwanadamu, lakini ina mahali pake pa kupumzika pa mwisho kwenye Mwamba usiotikisika wa Neno la Milele la Mungu.

<sup>12</sup> Neno! Ikiwa Mungu amelisema, hiyo ni Kweli milele. Kamwe hawezi kulighairi na kusema, “Sikulimaanisha.” Ninaweza kusema mambo nawe unaweza kusema mambo, kisha mara kwa mara tunayaghairi, kwa sababu tuliyasema kwa yote tuliyojua na kwa yote tuliyoweza. Lakini, basi, Mungu ni tofauti sana nasi. Yeye hana kikomo, kwa hiyo hasemi jambo moja isipokuwa liwe kamilifu kabisa. Kamwe haimlazimu kulighairi, kamwe hana haja ya kuomba msamaha kwa yale aliyosema. Daima linasimama, Kweli.

<sup>13</sup> Hata kwa Yesu, katika siku hizi kuu ambazo tunasherehekea, wakati Mungu alipomchinja Mwanawe kwa ajili ya dhambi za ulimwengu, labda ilikuwa maelfu ya miaka kabla hata msingi wa ulimwengu haujawekwa. Mungu alinena Neno, na ni bidhaa iliyokamilika Mbinguni wakati Mungu anapolinena; tayari limekamilika. Loo, laiti tungeweza tu kufahamu hilo linamaanisha nini, tungekuwa watu tofauti jinsi gani! Kuona katika Vitabu Vyake, hukumu ambazo zimewekwa humu kwa

ajili ya waasi, ingemfanya mtu kujichunguza mwenyewe, saa baada ya saa; na ingewafanya wenye haki kushangilia, saa baada ya saa, kusoma baraka ambazo Mungu amewaahidia walio waaminifu. Nasi tunaweza kuwa na hakika ya kwamba kila Neno litatimizwa, tuitie tu nanga nafsi yetu juu yake. Imekuwa hivyo sikuzote.

<sup>14</sup> Mungu alipozungumza na Nuhu, huko nyuma kabisa katika ulimwengu ulioitangulia gharika; pengine labda kabla Biblia haijapata kuandikwa, ama Biblia hii, kwa vyovyote vile, haijapata kuandikwa; Mungu alimwambia Nuhu dhoruba ilikuwa inakuja, nayo maji yangeifunika dunia. Na bila chembe moja ya ushahidi kwamba ingetokea, kila kitu kinyume sana, Nuhu akaondoka kwa hofu, akajenga safina, akaiweka tayari. Ilikuwa ni ya kumwokoa yeye na nyumba yake. Mungu kamwe hakumwaibisha, kwa maana lilikuwa ni Neno Lake. Ilibidi litendeke wakati Mungu aliposema lingetendeka.

<sup>15</sup> Sasa, wakati Ayubu, kile Kitabu cha kale sana katika Biblia, ambacho kiliandikwa labda kabla ya Mwanzo kuandikwa, nacho kikajumuishwa katika Biblia. Naye Musa akaandika Mwanzo. Ayubu, katika Kitabu chake, alitulia kwa uchaji juu ya ahadi Mungu aliyompa. Naye akasimama kando ya sadaka yake ya kuteketezwa, bila hofu moyoni mwake; akijua ya kwamba, yale Mungu aliyosema, Mungu aliweza kuyatimiza. Basi wakati kila kitu kilionekana kwenda kinyume, Ayubu alisimama imara kwa sababu ahadi ya Mungu ilikuwa thabiti. Mungu alimwahidi Ayubu, naye Ayubu akatulia juu ya ahadi hiyo.

<sup>16</sup> Loo, laiti kanisa lingeweza kufikia mahali hapo ambapo lingeweza kutulia kwa uchaji juu ya Neno la Milele la Mungu kuwa Kweli! Kungekuwa na tofauti jinsi gani, kungekuwa na marekebisho jinsi gani, kungekuwa na kukataliwa mbali jinsi gani, kungekuwa na furaha jinsi gani, kungekuwa na nguvu jinsi gani, wakati wanaume na wanawake wangemchukua Mungu juujuu, alichosema ni Kweli. Haijalishi hali ya mambo inaonekanaje, hiyo haina uhusiano nayo. Mungu alisema hivyo; hiyo inatosha!

<sup>17</sup> Naye Ayubu, alipokuwa katika wakati wa majaribu sana kwa ujuzi wake wote; wakati alipokuwa amepatikana, Mbele za Mungu, mtu mwenye haki. Hata Mungu alisema yeye alikuwa ni mkamilifu. Hapakuwapo na mtu kama yeye duniani. Ndipo Shetani akapewa majaliwa ya kumjaribu, akisema, “Nitamfanya akulaani mbele za uso Wako.”

<sup>18</sup> Naye karibu achukue uhai wa Ayubu, na angalifanya hivyo, lakini Mungu aliweka mpaka, akasema, “Unaweza kumfanyia lolote, ila usichukue uhai wake.”

<sup>19</sup> Ndipo Ayubu aliposimama kwenye majaribu ya wakati huo mgumu, alisema, “Ninajua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho Yeye atasimama juu ya nchi. Hata mabuu ya

ngozi yakiuharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu.” Haijalishi ilionekana kuwa giza jinsi gani, na jinsi ilionekana kuwa isivyo halisi, kulikuwa na kitu ambacho Ayubu alitia nanga nafsi yake juu yake, ahadi ya Milele ya Mungu. Loo, laiti tungaliweza kufanya hivyo! Angalieni, alitulia kwenye ahadi, “Najua Mkombozi wangu yu hai.”

<sup>20</sup> Nami nataka muone, kwa maneno ya usoni ninayotaka kusema, Ayubu alibainisha mahali pake pa kuzikwa. Ndipo Ayubu alipokufa, alizikwa hivyo.

<sup>21</sup> Kulikuwa na mtu mwingine, jina lake Ibrahimu, ambaye aliliamini Neno la Mungu. Naye alimwamini Mungu. Naye akayaita mambo yale yaliyokuwa kinyume na ahadi aliyopewa na Mungu, kana kwamba hayakuwapo. Aliliamini Neno la Mungu. Basi siku zilipopita, na majuma na miezi, na hata miaka ikapita, hilo kamwe halikumsumbua Ibrahimu hata kidogo. Biblia ilisema, “Hakusitasita, kwa kutokuamini, katika ahadi ya Mungu; bali alikuwa mwaminifu, akimtukuza Mungu.”

<sup>22</sup> Wakati kila kitu kilionekana, kila siku, kwa urahisi ilizidi kuwa ngumu kila siku; lakini badala ya kudhoofika, Ayubu aliimarika kila siku. Loo, ni hakikisho lenye baraka jinsi gani tulilo nalo! Wakati magumu yanapoonekana kuinuka kufanya hilo jambo, ambalo Mungu ameahidi, lisilowezekana; badala ya kutishika, kurudi ulimwenguni, inatupasa kusimama imara zaidi kuliko vile tulivyopata kusimama, juu ya BWANA ASEMA HIVI. Inapaswa kulimalizia, Mungu anaposema jambo fulani.

<sup>23</sup> Naye Ibrahimu akaviita vitu vilivyokuwako, kana kwamba havikuwepo, kwa sababu vilikuwa kinyume na Neno. Ndipo wakati Ibrahimu alipompoteza Sara, mpenzi wake na mke, baada ya miaka mingi ya kuishi pamoja, alinunua sehemu ya ardhi karibu na mahali ambapo Ayubu alizikwa, naye akamzika Sara. Unashangaa ni kwa nini? Walikuwa ni manabii! Waliona! Waliwasiliana na Mungu! Na sasa Ibrahimu alipokufa, alizikwa pamoja na Sara.

<sup>24</sup> Sasa, hakutaka jamaa hawa wampe sehemu hiyo ya ardhi. Aliinunua, mbele ya mashahidi. Ni mfano mzuri jinsi gani wa ubatizo. Aliinunua, mbele ya mashahidi, kwamba ilikuwa ni mali yake. Loo, hivyo ndivyo mwamini halisi anavyopaswa kuja, sio kuponyokea pembeni, bali kusimama mbele ya mashahidi, “Mimi ni shahidi wa Bwana Yesu, na wa Roho Mtakatifu, na wa kazi Zake kuu,” na zaidi sana tunapoona siku hii ovu ikikaribia.

<sup>25</sup> Halafu basi wakati mwana wa Ibrahimu, ambaye alikuwa Isaka, ile ahadi ilikuwa apewe yeye. Ndipo Isaka alipokufa, alizikwa pamoja na Ibrahimu. Naye Isaka akamzaa Yakobo.

<sup>26</sup> Naye Yakobo alipokuwa . . . alikufia mbali huko chini Misri. Lakini angalieni, kabla hajafa, alimwambia nabii mwanawe, Yusufu, “Njoo hapa, mwanangu, na uweke mkono wako juu ya nyonga yangu iliyolemaa.” Kwa maana kumbukeni jinsi

alivyokuwa mlemavu, ni kwa sababu Malaika wa Bwana aliigusa nyonga yake, akachechemea tangu siku hiyo na kuendelea. Alisema, “Weka mkono wako nyongani mwangu, uniapie kwa Mungu wa baba zetu, kwamba hutanizika huku chini Misri.” Kwa nini? Loo, walikuwa na Neno, walikuwa na ufunuo!

<sup>27</sup> Na hebu nikomee hapa, kusema ya kwamba kanisa la Mungu aliye hai limejengwa juu ya ufunuo wa Kiungu; si juu ya madhehebu, mashirika, si juu ya kanuni za imani ama mafundisho, bali juu ya Kweli iliyofunuliwa ya kiroho ya Mungu aliye hai.

<sup>28</sup> Habili, katika bustani ya Edeni, alikuwa nao wakati kanisa lilipoanza. Alijuaje kumleta mwana-kondoo? Kwa nini hakuleta tunda kama Kaini alivyofanya? Lakini ilifunuliwa kwake!

<sup>29</sup> Yesu akinena wakati mmoja, alisema, “Watu husema Mimi Mwana wa Adamu kuwa ni nani?”

“Wengine walisema Wewe ni ‘Musa,’ na ‘Eliya,’ kadhalika.”

Akasema, “Lakini ninyi mnasema Mimi ni nani?”

<sup>30</sup> Unaona, halitegemei kile mtu mwingine anachowazia, ni kile unachojua kuwa ni Kweli. “*Ninyi* mnasema nini?” Swali hilo lingemkabili kila mmoja wetu usoni usiku wa leo, “Wewe unasema nini?”

<sup>31</sup> Naye Petro akanena upesi, pasipo kusita hata kidogo, akasema, “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.”

<sup>32</sup> Kwa kuwa Yesu alijua siri za mioyo yote, kwa maana Yeye hakuwa mwingine ila Yehova aliyedhihirishwa katika mwili, basi Yeye akasema, “Heri wewe, Simoni, mwana wa Yona, kwa maana mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amefanya jambo hili. Na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haiwezi kulishinda.”

<sup>33</sup> Na sisi watu tunapoendelea, sisi Walutheri tunataka kutembea kwa imani, sisi Wamethodisti tunataka kupaza sauti tumpate, ninyi Wapentekoste mnataka kunena kwa lugha mumpate, lakini hiyo ni maili milioni kumi kutoka Kwake.

<sup>34</sup> Ni ufunuo wa Kiungu wa Bwana Yesu Kristo, ule Utu wa Uwepo Wake ukidhihirishwa moyoni, “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayatalishinda.” Inafanya kazi kikamilifu na Mathayo :24, 5:24, au, Yohana Mtakatifu 5:24, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele; wala hataingia hukumuni kamwe, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Si kwa sababu ulikuwa na tendo lolote, mhemuko wowote; lakini kwa sababu umekuwa na majaliwa ya Kristo kufunuliwa kwako kutoka Mbinguni, “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu.”

<sup>35</sup> Ndipo basi, Yakobo, alipokufa, mwanawe aliusafirisha mwili wake, naye akazikwa pamoja na Ibrahimu, Isaka, Sara, na Ayubu, katika Nchi Takatifu, huko Palestina.

<sup>36</sup> Halafu, Yusufu, akiwa nabii. Alifanikiwa huko Misri. Alimjua Mungu. Mungu alikuwa amejifunua Mwenyewe kwake. Basi alipokufa, alisema, “Msizike mifupa yangu huku chini, bali iwekeni . . . wakati . . . Siku moja hakika Mungu atawazuru!” Kwa nini? Alitulia kwa uchaji juu ya lile Neno la Mungu kwa Musa, “Miaka mia nne watalitumikia taifa hili, bali nitawatoa.” Alitulia kwa uchaji juu ya Neno.

<sup>37</sup> Basi ni kielelezo kizuri jinsi gani hapa, ikiwa utaangalia. Kila Mwebrania akipitia hapo, huku mgongo wake umecharazwa sana, na wanyapara wa watumwa. Basi alipoitazama hiyo mifupa ya nabii wake, Yusufu, alijua siku moja wataondoka. Kwa kuwa, mifupa hiyo iliachwa pale kama ukumbusho, ya kwamba siku moja wangeondoka.

<sup>38</sup> Imekuwa kama miaka kumi na mitano au kumi na minane iliyopita wakati Billy Paul, maskini yule mvulana mwenye umri wa yapata miaka mitano, hajaifikia hiyo . . . Tulikuwa na ua dogo tulilokuwa tukipeleka kwenye kaburi la mama yake, kwenye mapambazuko asubuhi moja, kwenye Pasaka, jua lilipokuwa tu likitokea, likichomoza; ama kabla tu ya mapambazuko, ndivyo ilivyokuwa, kisha twende ibadani. Basi tulipokuwa tukielekea kwenye kaburi, huyo jamaa mdogo akavua kofia yake huku tukisogea pale walipozikwa dada yake mdogo na mama yake. Ndipo akaanza kuguta na kulia, naye akasema, “Baba, mama yuko chini kule kwenye shimo lile?”

<sup>39</sup> Nikasema, “Hapana, mwanangu. Yeye hayuko chini kule kwenye shimo lile. Yeye ana hali bora zaidi mara milioni moja kuliko mimi na wewe.”

Akasema, “Je, nitamwona mama tena?”

<sup>40</sup> Nikasema, “Kwa neema ya Mungu, ukilitamani, unaweza kumwona tena.”

Kasema, “Je, mwili wake utawahi kutoka kwenye hili kaburi?”

<sup>41</sup> Nikasema, “Mpenzi, hebu funga macho yako, nami nitakusimulia hadithi ndogo. Mamia mengi ya miaka iliyopita, asubuhi ya leo, kulikuwa na kaburi lililoachwa tupu.” Nikasema, “Ni ukumbusho kwa ‘wale waliolala katika Mungu Kristo atawaleta pamoja Naye atakapokuja.’” Bila shaka yoyote, ninatulia kwa uchaji juu ya ahadi ya Milele ya Mungu!

<sup>42</sup> Kama vile Ayubu wa kale, tunaposikia ile “majivu kwa majivu, na mavumbi kwa mavumbi,” inanikumbusha kuhusu Longfellow, ambaye alisema:

Usiniambie, kwa nyimbo za maombolezo,  
 Maisha ni ndoto tupu tu!  
 Nayo nafsi imekufa inayolala,  
 Wala mambo hayako jinsi yanavyoonekana.

Yeye alisema:

Naam, maisha ni halisi! Maisha yana bidii!  
 Wala kaburi silo kikomo chake;  
 Kwa kuwa u mavumbi wewe, mavumbini  
 utarudi,  
 Haikunenwa juu ya nafsi.

<sup>43</sup> Wanauita thiofania, kwamba tunapoondoka hapa tunaingia mahali pengine. Popote pale, ninachukua Neno la yule mtume, aliposema, “Kama maskani hii iliyo ya dunia au makao yakiharibika, tunayo moja inayotungoja tayari, tutoke kwenye *hii* kuingia katika Ile.”

<sup>44</sup> Ibrahimu, Isaka, Yakobo, Ayubu, manabii wote, walitumaini na kuamini kwamba kulikuwako na ufufuo unaokuja, kwamba Mkombozi atakuja. Walitabiri habari Zake. Henoko alitabiri habari Zake; akatulia kwa uchaji, akautia muhuri ushuhuda wake kwake. Isaka, Yakobo, Danieli, Yeremia, Ezeieli, walitulia kwa uchaji juu ya wakati ambao Masihi angekuja.

<sup>45</sup> Nao wakafa na nafsi zao zikaingia Paradiso. Wasingeweza kwenda Mbele za Mungu, kwa sababu (tulikuwa nalo jana usiku) kwamba damu ya mafahali na mbuzi isingeweza kusamehe dhambi; ilifunika tu dhambi, ikinena juu ya siku ambapo ile Dhabihu kamilifu; maana damu katika yule mnyama haikuweza kumrudia mwabuduo, kwa kuwa basi asingeacha kutoa dhabihu za aina hiyo.

<sup>46</sup> Lakini Mwana wa Mungu alipokufa, ule Uhai uliokuwa ndani Yake haukuwa mwingine ila Mungu, kurudi na kutuasili katika familia ya Mungu. Na sasa sisi ni watoto wa Mungu, ule Uhai kutoka kwa Damu Yake.

<sup>47</sup> Sasa angalieni upesi, tunapofuata. Wakati huko nyuma katika Agano la Kale, na wale walioamini na kuabudu, na kufa katika Imani, wakiungojea wakati huo. Sababu ya manabii hao kufanya hivyo, na kutaka kuzikwa kule Palestina, walijua kwamba ufufuo hautakuwa Misri. Utakuwa Palestina, peke yake.

<sup>48</sup> Ndio maana nasema usiku wa leo: Nina kila aina ya majina; sijali watu wananiita nini, hilo halimaanishi kitu kwangu. Jambo pekee ninalotaka kufanya, ni kujua hili, ya kuwa nimekufa, na uhai wangu umefichwa ndani ya Kristo, kwa njia ya Mungu, na kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu; kwamba atakapoita miongoni mwa wafu, nitajibu siku hiyo. Nizikeni katika Kristo, kwa maana wale walio ndani ya Kristo Mungu atawaleta pamoja Naye siku hiyo.

49 Je, tunaingiaje ndani ya Kristo? Wakorintho wa Kwanza 12:13, “Kwa Roho mmoja sisi sote tunabatizwa kuwa Mwili mmoja, na kuwa raia wenzi wa Ufalme wa Mungu.” Tunakiri kuwa wasafiri na wageni katika dunia hii, tena, hatuyatafuti mambo haya ya kilimwengu, bali tunakutazamia kuja kwake Mfalme aliyebarikiwa kuitwaa milki hii, toka bahari hata bahari isiyo na mipaka, atakapokuja katika utukufu Wake. Bila shaka, tunakutazamia Kuja Kwake.

50 Halafu hakuna shaka niani mwangu, lakini hayo ndiyo Yesu alikuwa nayo niani Mwake alipokuwa hapa duniani, yalikuwa ni huko kutoweza kukosea kwa Neno la Milele la Mungu. Kwa maana, tunajua ya kwamba ndani Yake mlikaa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya Mwili. Uungu wote ulikuwa ndani Yake. Alikuwa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu pia, bali aliishi katika umbo la mwanadamu; ile thiofania ya Mungu, ule mfano mkuu wa Mungu aliomfanyizia mwanadamu, kisha akamweka duniani. Alikuwa na mwili. Mungu hayuko bila mwili. Mungu anao mwili, nao unaonekana kama mwanadamu. Musa aliuona, wengine waliuona, nao unaonekana kama mwanadamu.

51 Na ni sura tu, *hii* ndiyo, ya kile Ule ulicho. Na kila kitu duniani, uzuri, utamu, uzuri wa dunia, si kitu kingine ulimwenguni ila ni jibu la kilicho bora kuliko hicho, ambacho kinatungojea tunapouacha ulimwengu huu. Kwa maana, kila kitu duniani ni mfano tu wa kile kilicho Mbinguni. Kila kitu kizuri, kila kitu ambacho ni cha haki, kila kitu kinachovutia, miti, ndege, kila kitu, ni mfano tu wa kile kilicho Mbinguni.

52 Maisha yetu yenyewe ni mfano tu. Ni kivuli tu, wala sio kitu halisi. Ni upande hasi. Inahitaji kifo kuisafisha hiyo picha, kuturudisha katika thiofania tulimotoka. Ndipo katika ufufuo tunakuja katika sura Yake, mwili uliofufuliwa. Ni mzuri jinsi gani; sio tu mzuri, bali ni halisi, Ukweli mnyofu wa Neno la Mungu la Milele, kwamba tutakuwa kama Yeye.

53 Angalieni sasa, Yesu, aliyekabidhiwa nguvu zote za Mungu, lakini, wakati alipokutana na Shetani, hakutumia nguvu Zake zozote. Alirejea tu kwenye Neno! Alirejea. Alisema, “Imeandikwa, ‘Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.’”

54 Basi unawezaje kusema unaweza kukaa nyumbani na kuwa Mkristo mzuri kama vile ungekuwa kanisani? Huwezi kuwa. Soma Neno! Roho Mtakatifu hula Neno. Biblia ni chakula cha kiroho cha Mungu kwa Kanisa Lake. Naye Roho Mtakatifu Ndiye anayelileta kwako na kuliweka moyoni, na kwa shukrani unalinyunyizia maji. Na kila ahadi ya Kiungu itazaa kile tu hasa Mungu alisema ingezaa. Haina budi kuzaa. Ni Neno Lake, na ni Uzima.



55 Sasa, nilikuwa nimesahau kwamba nilipaswa kutumia nusu saa pekee. Inanichukua muda mrefu sana kufikia kile ninachotaka kusema.

56 Lakini mwangalieni Yesu katika ile saa moja au mbili za mwisho, za maisha Yake, unabii mwingi, mwingi sana ulitimizwa.

57 Mtu fulani aliniambia, “Ndugu Branham, *hili* halina budi kutukia, na *lile* halina budi kutukia.”

Nikasema, “Yanaweza kutukia katika saa moja.”

58 Ikiwa utasoma Zaburi ya 22, halafu basi uitazame saa Yake ya kufa msalabani, ninasahau tu sasa ni unabii ngapi mkuu uliotimizwa katika saa mbili au tatu za mwisho za maisha Yake! Bila shaka, “Waliichoma miguu Yangu na mikono Yangu. Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha?” na kadhalika, kama vile Daudi alivyolia.

59 Na halafu jambo lingine ninalotaka muone, ile Kweli, ile sehemu isiyokosea ya Neno la Mungu. Biblia ilisema, “Anahifadhi mifupa yake yote, hakuna hata mmoja uliovunjika.” Kwa maana katika mfano, mwana-kondoo wa pasaka alikuwa ni mfano wake. Huyu Mwana-kondoo hapaswi kuwa na doa, hakuna mifupa iliyovunjika inayoweza kuwa ndani ya huyo mwana-kondoo. Na saa ile alipokuwa... Alipokuwa amekufa, walipanda wakaivunje miguu Yake kwa nyundo. Na kabla tu... Tazama wakati huo muhimu sana! Yule mtu mwenye nyundo, akiwa tayari kuitwanga miguu Yake, lakini Neno la Mungu lilisema, “Hakuna mfupa mmoja utakaovunjwa katika mwili Wake.”

“Je, itakuwaje?” Tunakuwa na haraka.

60 Neno la Mungu ni la Milele! Ikiwa Neno la Mungu ni kamilifu hivyo, hao walio ndani ya Kristo wana hakika kufufuka kadiri kulivyo na ufufuo. Mungu anawajibika vivyo hivyo kwa Neno Lake, kukuponya, kadiri awajibikavyo kukuokoa. Kwa maana, Yeye, Neno Lake ndilo lililoahidi jambo hilo. Ni Neno la Mungu, nasi hatuna haki ya kuondoa Kwake. Bali kusema tu, “Ni Kweli.” Liaminini! Haidhuru kinachotokea, liaminini, kwa vyovyote vile. Hivyo ndivyo iliwabidi wengine wao kuliadini, nasi hatujatengwa na jambo hilo. Mungu aliwapa Israeli Palestina, lakini iliwabidi kupigania kila inchi ya ardhi waliyopata. Ahadi ni yako, lakini unapaswa kupigania kila inchi unayodai; ibilisi atahakikisha hilo, bila shaka atahakikisha umeipigania.

61 Lakini angalia walipokuwa tayari kuivunja miguu ya Bwana wetu Yesu, kama nyundo hiyo ingaliupiga mguu na kuuvunja, Mungu angeonekana kuwa mwongo. Lakini hapakuwa na pepo wa kutosha katika mateso yote ya gizani kuiruhusu nyundo hiyo ipige mwili huo wa thamani. Kwa maana Daudi, miaka mia nane kabla ya wakati huo, alisema, “Hakutakuwako na mfupa mmoja

utakaovunjwa katika mwili Wake.” Neno la Mungu halina budi kusimama likiwa Kweli.

<sup>62</sup> Lakini walifanya nini basi? Walichukua mkuki na kuuchomeka ubavuni Mwake, ndipo Damu na maji yakatoka, kutimiza yale ambayo Biblia ilisema, “Waliichoma mikono Yangu na ubavu Wangu.” Neno lilitimizwa.

<sup>63</sup> Sasa wakati alipokuwa akifa, loo, ilikuwa ni saa ya kuogofya jinsi gani! Ninauwazia wimbo ule, na, kusema kweli, unanifanya tu kujisikia vibaya sana, ninapouwazia ule wimbo ambao mshairi aliuandika miaka mingi iliyopita.

Kati ya miamba inayopasuka na mbingu zenye  
giza,  
Mwokozi wangu aliinamisha kichwa Chake na  
akafa;  
Pazia lililofunguliwa liliifungua njia  
Kuziendea furaha za Mbinguni na siku isiyo na  
mwisho.

<sup>64</sup> Naye alipokuwa amening’inia pale, akivuja damu na kufa, alipokiinamisha kichwa Chake, jua lilijionea aibu sana, kuvitazama viumbe vipatikanavyo na mauti ambavyo Mungu aliviumba kwa mfano Wake, ingemlazimu kulipa gharama kama hiyo ili kuvikomboa, jua lilikataa kutazama chini duniani katika saa hiyo. Mwezi uliona aibu sana hata akahama mahali pake. Nazo nyota zikaipa dunia kisogo. Jinsi hapana budi dhambi ni kitu cha kuchukiza sana! Jinsi ilivyomlazimu Mungu kuishughulikia!

<sup>65</sup> Na kuwaona hao makuhani wenye kudhihaki, huku mate yakining’inia usoni Mwake. Mtu mmoja akamchapa kichwani, kwa mwanzi, akasema, “Ikiwa Wewe ni Nabii, tuambie ni nani aliyekupiga.” Mmoja wao akang’oa ndevu usoni Mwake, na kumchapa kofi usoni, naye alimtaka ajitetee.

<sup>66</sup> Akasema, “Kama Ufalme Wangu ulikuwa wa ulimwengu huu, mara moja ningemwita Baba Yangu, angenitumia Mimi majeshi kumi na mawili ya Malaika.”

<sup>67</sup> Ingeweza kubadilishwa, lakini angeweza kufanya hivyo? Kamwe asingeweza kufanya hivyo, kwa maana ilikuwa ni watoto Wake mwenyewe wakiililia Damu Yake. Ungeweza kuwazia dadi, baba, pamoja na watoto wake mwenyewe (gizani) wakilia waimwage damu ya baba yao mwenyewe? Hiyo ndiyo sababu asingeweza kufanya lingine ila kufa. Kama hakufanya hivyo, ilikuwa ni maangamizi kwa watoto Wake, ilikuwa ni maangamizi kwa hao viumbe. Bali ilimbidi kufa, kuwaokoa watu Wake.

<sup>68</sup> Basi alipokufa, alipoinamisha kichwa Chake, maskini dunia hii ilipata mtetemeko uliopitia mgongoni mwake. Hapana shaka ilishikwa na fadhaa ya unyong’onyevu, kwa maana Biblia ilisema kwamba “dunia nzima, tangu saa sita hadi saa

tisa, ilikuwa giza, kilichokuwa juu ya uso wote wa dunia.” Nayo dunia ikatetemeka, na miamba ikapasuka. Nalo pazia la hekalu likapasuka kutoka juu hata chini; bloku za dhabihu zikapinduliwa. Mwana wa Mungu aliye hai akafa. Alikuwa mfu sana mpaka jua likatambua. Alikuwa mfu sana mpaka mwezi ukatambua. Alikuwa mfu sana hata nyota zikatambua. Alikuwa mfu sana hata dunia ikatambua. Alikuwa mfu sana hata viumbe vikatambua, angahewa ikatambua. Kila kitu ilibidi kujua huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu! Kwa kuwa, Neno la Mungu halingeweza kushindwa, aliahidiwa, tangu bustani ya Edeni, “Uzao ambao ungekiponda kichwa cha nyoka.”

69 Sasa ilikuwaje Kwake? Alienda wapi alipouacha msalaba na kwenda kwenye kaburi la Yusufu wa Arimathaya?

70 Alikuwa maskini sana hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake. Alizaliwa kwenye hori, akiwa na jina baya sana nyuma Yake, kama “mtoto haramu.” Alichekwa, akadhahiwa, akadharauliwa, duniani. Alifanyiwa mzaha, na kukataliwa. Na alipokufa, ilimbidi kufa kwa adhabu ya kifo, kati ya wezi wawili. Na hakuwa hata na mahali pa kuzikiwa, ndipo akazikwa kwenye kaburi la mtu mwingine. Mungu yeye yule wa Mbinguni akija duniani! Kwani tunafikiri sisi ni nani, ambao inatupasa kupitia mateso kidogo? Alichotufanyia sisi! Liwazie, rafiki, lichunguze.

71 Yule askari wa Kirumi alisema, “Kweli, huyo ni Mwana wa Mungu.” Ilimbidi mwenye dhambi kulitambua. Yuda alisema, “Nimeisaliti Damu isiyo na hatia.” Ilibidi aitambue. Dunia nzima ikaitambua.

72 Basi alienda wapi? Mtu akifa, je, hilo huishia hapo? La, bwana. Ilimbidi afe jinsi hiyo kwa sababu Biblia ya Mungu ilisema ya kwamba angekufa hivyo. Naye aliamini Neno la Mungu. Hiyo ndiyo sababu angeweza kusema, katika maisha Yake, “Livunjeni hekalu hili, nami nitalisimamisha katika siku tatu.”

73 Kwa maana Daudi alisema, mahali pamoja tu, katika Biblia, chini ya uvuvio, wakati Daudi, mtu wa Mungu, nabii aliyetiwa mafuta kwa Neno, aliposema, “Sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu, wala sitaiacha nafsi Yake katika kuzimu.”

74 Yesu alisema, “Uharibuni mwili huu, nami nitaufufua katika siku tatu.” Alijua ya kwamba Neno la Mungu lisingeweza kushindwa. Loo, jamani!

75 Kama angaliweza kutulia kwa uchaji juu ya hilo, akiamini ya kwamba Neno la Mungu lisingeweza kushindwa, ni zaidi sana jinsi gani tunavyoweza kutulia kwa uchaji kwamba tumezaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu, Naye ni shahidi moyoni mwetu sasa hivi kwamba tunajua ya kwamba Mkombozi wetu yu hai na atakuja tena siku moja. Uwe na hakika kwamba wale walio ndani ya Kristo Mungu atawaleta pamoja Naye! Sasa angalia.

<sup>76</sup> Huyo hapo. Alijua kwamba hakuna chembe hata moja ya mwili huo ingeharibika. Saa sabini na mbili, uharibifu unaingia. Hiyo ndiyo sababu Yeye hakukaa siku hizo tatu. Alikufa Ijumaa alasiri, akafufuka Jumapili asubuhi. Lakini, ilikuwa ndani ya hizo siku tatu. Ndani ya siku hizo tatu alipaswa kufufuka tena, kwa maana alilitumaini Neno la Mungu.

<sup>77</sup> Huyu hapa anaenda! Aliondoka wapi alipoondoka? Biblia ilisema, “Alipaa juu. Akaenda na kuzihubiri nafsi zilizokuwa kifungoni, ambazo hazikutubu katika uvumilivu wa siku za Nuhu.” Nafsi Yake, Roho Yake, thiofania Yake ya utu Wake Mwenyewe, ilishuka. Hebu tumfuate Yeye. Je, ungependa, usiku wa leo, kumfuata Yeye kwa dakika chache? Hebu tuone alikokwenda.

<sup>78</sup> Chini kidogo tu ya maeneo ya viumbe vya kibinadamu kunayo milki ya nguvu za pepo; chini ya hapo. . . juu tu ya hapo zinakaa nafsi za wadhalimu; chini yake mnakaa milki yenyewe ya Shetani, kuzimu. Kisha juu yetu tu anakaa Roho Mtakatifu; kisha chini ya Madhabahu zimo nafsi za wenye haki; anayefuata ni Mungu Mwenyewe. Moja inashuka chini, moja ikipanda juu; roho hizo mbili ziko duniani, zikiwashawishi watu wa dunia hii.

<sup>79</sup> Basi Yesu alipokufa, anapanda juu, chini kule. Ninaweza kumwona Ijumaa hiyo alasiri, baada ya kufa Kwake, [Ndugu Branham anagonga—Mh.] anabisha mlango wa maeneo ya waliopotea. Hebu tumfuatilie kwa dakika moja. Mlango unafunguka. Kulikuwako na wanawake, kulikuwa na wanaume, kulikuwako na wasichana, kulikuwako na wazee, wote walikuwa pamoja katika eneo hilo la kutisha liitwalo gereza la watu waliopotea.

<sup>80</sup> Kama ningalikuwa na wakati, ningependa kuwaambia. Na linaweza likawa ni ono tu. Lakini wakati mmoja nilizuru mahali hapo, na kupiga mayowe nikiomba rehema, nilipokuwa mwenye dhambi nikifanyiwa upasuaji. Nilipojirudia, nilikuwa nimesimama Magharibi, nimeinua mikono yangu kuelekea Mbinguni, na msalaba ukiniangazia.

<sup>81</sup> Lakini katika mahali hapo pa maombolezo, Yesu alikuja mlangoni. Kila kitu ilibidi kishuhudie kwamba Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu, kwa sababu walikuwa wamehubiriwa katika uvumilivu wa siku za Nuhu. Akabisha mlangoni, akasema, “Mimi Ndiye Ambaye Henoko alinena habari zake. Mimi ndimi ule Uzao wa mwanamke, ambaye alikuwa atakiponda kichwa cha nyoka. Kila Neno la Mungu limetimizwa; ndio kwanza nife pale Kalvari, nami nimelinunua Kanisa Langu. Na Yule ambaye Henoko alinena habari zake, Mimi Ndiye.” Nao walikuwa bila rehema, bila tumaini, kwa sababu walikuwa wameasi. Na mlango ukafungwa mbele zao.

<sup>82</sup> Akashuka kwenye maeneo ya pepo! Moja kwa moja kwenye malango yenyewe ya kuzimu! Akaubisha mlango. [Ndugu Branham anagonga—Mh.]

<sup>83</sup> Huu ni wakati alipokuwa kaburini, mwili Wake ukiwamo humo, ukingojea ufufuo. Alitembelea sehemu ambazo wenye haki na wasio haki huenda; ambapo utakwenda moja ya siku hizi, mahali pamoja ama pengine.

<sup>84</sup> Naye anabisha kwenye mlango wa kuzimu. [Ndugu Branham anagonga—Mh.] Na, alipofanya hivyo, ibilisi akatokea. Nami ninaweza tu kumsikia akisema, “Loo, kwa hiyo hatimaye ulifika. Hakika nilifikiri nilikupata Wewe nilipomwua Habili.”

<sup>85</sup> Unaona, wakati Uzao huo ulipoahidiwa katika bustani ya Edeni, ibilisi daima amejaribu kuuangamiza Uzao huo. Nacho kifo cha Habili, na kule kuja kwa Sethi, kulikuwa tu ni kufa, kuzikwa, na kufufuka kwa Kristo. Uzao huo hauna budi kuendelea. Naye alijaribu kuuangamiza.

<sup>86</sup> Akasema, “Nilifikiri nilikupata Wewe nilipomwangamiza Habili. Nilidhani nilikupata nilipowaangamiza manabii. Nilikuwa na hakika kwamba nilikupata nilipomkata kichwa Yohana. Lakini sasa, hata hivyo, umefika. Nimekupata sasa.” Loo, jamani!

<sup>87</sup> Ninaweza kumsikia akisema, “Shetani, njoo hapa!” Yeye ni Bosi sasa. Ananyosha mkono, anaunyakua ule ufunguo wa mauti na kuzimu kutoka ubavuni mwake, akauning’iniza ubavuni Mwake Mwenyewe. “Ninataka kukupa notisi. Umekuwa laghai muda mrefu kutosha. Mimi ni Mwana wa Mungu aliye hai niliyezaliwa na bikira. Damu Yangu ingali imelowa msalabani, na deni kamili limelipwa! Huna haki tena. Umenyang’anywa zote. Nipe funguo hizo!” Hiyo ni kweli. Akageuka na kumpiga teke zuri kwelikweli, na kuufunga mlango, na kusema, “Baki humo ndani! Mimi ndiye Bosi tangu sasa na kuendelea.”

<sup>88</sup> Sasa, Yeye hakuwa na funguo za Ufalme, maana alimpa Petro; tutapata hayo yote asubuhi, katika ubatizo wa maji. Lakini alikuwa na funguo za mauti na kuzimu, Naye akazinyakua; baada ya kufufuka Kwake, alisema, “Ninazo funguo za mauti na kuzimu.” Petro alikuwa na funguo za Ufalme. Shetani alikuwa na funguo za mauti na kuzimu; lakini sasa Yesu anazo, Yeye ndiye Bosi.

<sup>89</sup> Huyu hapa anaanza. Inakaribia Pasaka; muda unaenda kasi. Lakini kuna kundi lingine. Yu wapi Ayubu? Ibrahimu yuko wapi? Wako wapi? Wako wapi wale jamaa walioliamini Neno la Mungu? Je, amewasahau? Je, kifo kiliwaangamiza? Je, hakukuwa na lingine? Hasha, hashu; Mungu hana budi kulitimiza Neno Lake.

<sup>90</sup> Ninaweza kumwona. Hebu tuchungulie kidogo Paradiso, na tutazame kule. Basi namwona Sara na Ibrahimu wakizunguka pale, na baada ya kitambo kidogo [Ndugu Branham anagonga—

Mh.] kitu fulani mlangoni. Ibrahimu anaenda na kufungua mlango, kasema, “Mpenzi, njoo hapa. Angalia hapa! Angalia hapa, yule ndiye Yule yule aliyesimama pamoja nami chini ya mwaloni siku ile.” Yeye ni Mungu wa Ibrahimu.

<sup>91</sup> Wakati uo huo tu naweza kumwona Danieli akitazama juu ya bega lake, na kusema, “Yule ndiye lile Jiwe lililokatwa mlimani, hakika kama ninavyosimama hapa.”

<sup>92</sup> Namwona Ayubu akisimama, akasema, “Huyo ni Mkombozi wangu ambaye nilisema ninajua yu hai, na siku moja angesimama juu ya nchi. Huenda mwili wangu ukawa si zaidi ya kijiko kidogo cha majivu, lakini katika dakika kumi na tano tangu sasa nitakuwa ndani yake tena. Huyo Ndiye.”

<sup>93</sup> Ezekieli anatazama huko juu, na kusema, “Nilimwona Mtu huyo huyo kama Gurudumu katikati ya Gurudumu, likizunguka, juu sana katikati ya hewa.” Loo, jamani!

<sup>94</sup> Kisha Henoko anatokea. Henoko alisema, “Nilimwona akija na maelfu kumi ya watakatifu Wake, kufanya hukumu.”

<sup>95</sup> Hao hapo watakatifu wa Agano la Kale walingoja, hakika walingoja, chini ya upatanisho wa damu. Hawangeweza kwenda Mbele za Mungu, Mungu wa Mbinguni, kwa sababu damu ya mbuzi na kondoo haingeweza kuondoa dhambi.

<sup>96</sup> Lakini akasema, “Ndugu zangu, mimi ndiye Yule mnayenifikiria kuwa. Mimi ndiye ule Uzao wa mwanamke. Mimi ni Mwana wa Daudi. Mimi ni Mwana wa Mungu. Mimi Ndiye niliyezaliwa na bikira. Damu Yangu imefanya upatanisho kwa ajili yake. Mlingoja chini ya damu ya kondoo na mbuzi, lakini sasa Damu Yangu inapatanisha, nanyi mko huru. Haya twendeni juu, inakaribia Pasaka.” Hebu wazia, hiyo ilikuwa tu yapata miaka elfu moja mia tisa na kitu iliyopita, usiku wa leo.

<sup>97</sup> Naweza kumsikia Ibrahimu akisema, “Bwana, tutakaposimama katika miili yetu tena; nami pamoja na Sara tuliipenda sana; je, utajali tukisimama kidogo, kwa namna fulani, njiani Mwako?”

<sup>98</sup> Vema, ninaweza kumsikia akisema, “Mbona, hapana, bila shaka hapana. Nitakaa pamoja na wanafunzi Wangu kama siku arobaini. Angalieni kote muone jinsi kila kitu kinavyoonekana!”

<sup>99</sup> Katika asubuhi hiyo tukufu ya Pasaka (ambapo tutaanzia asubuhi, Bwana akipenda) alipofufuka kutoka kwa wafu, Biblia ilisema, kulingana na Mathayo Mtakatifu 27, ya kwamba “Wengi wa watakatifu waliolala katika mavumbi ya nchi, walifufuka na kutoka makaburini.” Ilikuwa ni akina nani? Ibrahimu, Isaka, Yakobo, Ayubu, wale ambao kwa ufunuo uliofunuliwa wa kiroho walijua ya kwamba Mkombozi angesimama duniani siku moja. Hao ndio, malimbuko ya wale waliolala. Huko wakatembea

mjini. Ninaweza kuwaona Sara na Ibrahimu, wachanga, na wamejaa . . . na warembo, na—na wachangamfu sana, wasizeeke tena, wasiwe wagonjwa tena, wasione njaa tena, wakitembea katika miili yao.

<sup>100</sup> Kayafa akisimama pale, akisema, “Mnajua nini? Kuna jambo lililotokea hivi majuzi, angalieni tu machafuko haya hekalu hilo lililomo! Kuna . . . Itabidi tumtafute mtu wa kushona pazia hilo. Hebu angalieni hayo, sanduku la dhabihu limepinduliwa. Nini kilitokea? Kwani Jamaa huyo alikuwa mnajimu? Alikuwa mchawi? Au, ilikuwaje? Aisee! Njoo hapa, Josephus, ni nani wale mume na mke vijana wanaosimama pale?”

Ibrahimu akasema, “Sara, tumetambulikana. Afadhali tutoke nje.”

<sup>101</sup> “Wakawatokea wengi!” Si hayo tu. Katika kufunga, angalieni. Siku moja baada ya Yeye . . . walikuwa wametembelea; Ibrahimu, Isaka, Yakobo, na wote hao walikuwa wameitembelea nchi ya uenyaji wao. Yesu alipopaa juu . . .

<sup>102</sup> Unasema, “Ndugu Branham, hiyo ni hadithi ya kubuni?” Hapana, bwana! Nitawaonyesha katika Maandiko, katika dakika moja.

<sup>103</sup> Alipoanza kupanda juu, walimwona Yeye tu, bali watakatifu wa Agano la Kale walikwenda pamoja Naye, kwa maana Biblia ilisema kwamba “Aliteka mateka, na kuwapa wanadamu vipawa.” Nami ninaweza kumwona anapopaa juu, na kujiunga na kanisa Lake.

<sup>104</sup> Malaika wawili kutoka kwenye bendi iliyokuwa ikicheza muziki, walirudi pale, na kusema, “Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama juu? Kwa maana Yesu yuyu huyu, aliyechukuliwa juu, anakuja tena.” Bila shaka! Wakarudi upesi wakajiunge na msafara huo.

<sup>105</sup> Ndipo moja kwa moja Yesu na watakatifu wa Agano la Kale wakapitia angani. Wakapita mwezi, wakapita jua, wakapita nyota. Ndipo walipokaribia Mbingu hizo nzuri, nyeupe, watakatifu wa Agano la Kale wakapiga makelele, wakiyanukuu Maandiko, “Inukeni, enyi malango ya milele, na inukeni! Inukeni, enyi malango ya milele, inukeni! Ndipo Mfalme wa Utukufu aingie!”

<sup>106</sup> Malaika wote wakakusanyika juu ya mihimili ya Mbinguni, wakasema, “Ni nani huyu Mfalme wa Utukufu?”

<sup>107</sup> Watakatifu wa Agano la Kale wakasema, “Bwana wa majeshi, hodari wa vita! Alikuwa Mshindi!”

<sup>108</sup> Malaika akakibonyeza kile kitufe kikubwa, nayo malango ya lulu yakafunguka.

<sup>109</sup> Moja kwa moja kupitia Jiji la Yerusalemu akaja yule Mshindi mkuu, mwenye nguvu, akiwaleta watakatifu wa Agano la Kale.

Bendi za Malaika zikicheza, huku Malaika wakipiga makelele. Alikuwa Mshindi mwenye nguvu! Alikuwa na funguo za mauti na kuzimu zikining'inia ubavuni Mwake, akishuka moja kwa moja kupita yale majumba ya Utukufu mpaka akafika kwenye kile Kiti cha Enzi. Naye akasema, "Baba, hawa hapa. Waliadini, kwa imani katika Neno Lako, ya kwamba ningekuja siku moja. Nimeshinda mauti na kuzimu pia." Ilikuwa ni nini, ndugu? Alikuwa na makovu mkononi Mwake, kuonyesha ya kwamba alikuwa kwenye vita. Utukufu kwa Mungu aliye Juu sana! Yeye ndiye yule Mshindi mkuu! "Hawa hapa, Baba; Ibrahimu, Isaka, na Yakobo."

<sup>110</sup> Ninaweza kumsikia akisema, "Mwanangu, panda huku juu kando Yangu, ukaketi hata nikapomfanya kila adui kuwa chini ya miguu Yako." Ndugu, siku moja atakuja tena, nayo itakuwa siku ya jinsi gani!

<sup>111</sup> Hakupumzika alipokuwa kaburini. Tunafikiri alikuwa amelala tu pale, maiti. Lakini alikuwa huko chini angali akishinda, alishuka na kumnyang'anya Shetani funguo, Yeye anazo funguo za mauti na kuzimu pia, usiku wa leo. Alisema, "Kwa kuwa Mimi ni hai, mnaweza kuwa hai, pia."

<sup>112</sup> Nashangaa usiku wa leo, ndugu yangu mpendwa, dada, umeliwazia hilo kwa uaminifu? Je, unatambua kwamba unaishi tu kwa sababu Yeye yu hai? Je, umeithamini vya kutosha kujitolea, na kusema, "Mungu, mimi hapa, mwenye dhambi, unirehemu"? Je, umewahi kuikubali hiyo Sadaka itoshelezayo kwa yote? Je, umewahi kumwambia kuwa ulimpenda? Je, inaduru hisia zako unapofanya makosa? Ikiwa hujawahi kuufikia ujuzi huo sasa, katika kuzikwa huku! Ambapo, wakati wetu unaenda. Tunajisikia vizuri tu! Lakini, nashangaa, kama hujapata kumpokea Kristo kama Mwokozi wako binafsi, sijui kama ungefanya hivyo tunapoinamisha vichwa vyetu kwa muda mfupi katika maombi mafupi.

<sup>113</sup> Cheza huo, *Kati ya Miamba Inayopasuka*, tafadhali, Dada Gertie, kama unao. Vema, wowote ule utafaa.

<sup>114</sup> Huku vichwa vyenu vimeinamishwa, nitawauliza swali la moyoni sana. Kumbukeni marafiki, mwenye dhambi au mtakatifu, hujakoma kuwepo tunapokuzika. Nafsi yako iko mahali fulani. Sasa, Yesu alipatembelea mahali hapo pawili, kulingana na Maandiko. Angekupata wapi kama ungeondoka usiku wa leo? Je, ungefungiwa mlango wa rehema mbele zako, kwa sababu umekataa? Kumbuka, si kwamba tu Yeye ni Mwokozi, Yeye ni Hakimumu. Wewe ndiye mwamuzi sasa, unamchukuliaje? Mwache awe Mwokozi wako sasa.

<sup>115</sup> Hadithi ndogo inakuja akilini mwangu. Siku moja mvulana mdogo alikuwa ameketi katika m—mkokoteni. Bunduki ikafyatuka chini mtaani, nao farasi wakakimbia, alikuwa akipita juu ya jabali. Kaoboi mdogo akakimbia na



kuwasimamisha farasi kabla tu ya huo mkokoteni kupita juu ya hilo jabali, maana ulikuwa na mtoto mchanga ndani yake. Akayaokoa maisha ya huyo mtoto mchanga.

<sup>116</sup> Miaka mingi baadaye, alisimama mahakamani. Mvulana yuyu huyu alikuwa amefanya uhalifu, akachukua njia mbaya, akawa na hatia. Alikuwa akinywa pombe, akicheza kamari, akampiga mtu risasi; naye akawa na hatia, akapatikana na hatia. Ndipo hakimu akasimama na kusema, “Ninakuhukumu kunyongwa kwa shingo yako hata maisha yako ya kibinadamu yatakapokwisha.”

<sup>117</sup> Yule kijana akasema, “Hakimu!” Naye akavunja utaratibu wa mahakama, aliporuka juu ya chuma na kuanguka miguuni pa hakimu, akiomba rehema. Akasema, “Hakimu, hebu utazame uso wangu! Hivi hunijui?”

Alisema, “Hapana, mwanangu, sikujuui.”

<sup>118</sup> Akasema, “Unayakumbuka maisha ya mvulana fulani mdogo uliyoyaokoa, miaka mingi iliyopita, kutoka kwa farasi aliyetoroka?”

Akasema, “Naam, nakumbuka.”

<sup>119</sup> Akasema, “Mimi ndiye mvulana huyo.” Akasema, “Hakimu, uliniokoa wakati huo. Niokoe sasa!”

<sup>120</sup> Hakimu akainama akamtazama, akasema, “Mwanangu, siku hiyo nilikuwa mwokozi wako. Leo hii mimi ni hakimu wako.”

<sup>121</sup> Leo Yeye ni Mwokozi wako, ewe mwenye dhambi, kesho huenda akawa ni Hakimu wako. Hebu tuliwazie sasa, muziki unapocheza. Na kila mtu akiomba, wale walio kwenye maeneo ya maombi pamoja na Mungu.

<sup>122</sup> Nashangaa usiku wa leo sasa, upesi, wale ambao wangependa kumpokea Kristo kama Mwokozi wa binafsi, useme, “Mungu, unirehemu, mwenye dhambi. Ninataka kuja kwa Damu iliyomwagika. Nimechoka na kujiunga na makanisa na kukimbia mahali mahali. Nataka kuzaliwa mara ya pili. Ninataka ujuzi moyoni mwangu ambapo ninajua kwamba Kristo amejifunua Mwenyewe kwangu, kwa ufunuo wa kiroho uliounena hivi punde, Ndugu Branham. Nataka huo ufunuo wa kiroho, Roho Mtakatifu moyoni mwangu, akinifanya kuwa hai, akimfanya Kristo halisi zaidi kwangu kuliko nilivyo kwa nafsi yangu. Ninatamani ujuzi huo, Ndugu Branham. Je, utaniombea ninapoinua mkono wangu?” Je, utainua mkono wako sasa, ambaye unatamani kukumbukwa. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki huko nyuma, mama. Hilo ni jema. Mungu akubariki, bwana. Hilo ni jema. Inua mikono yako, sasa endelea kupanda juu pamoja na mkono wako.

<sup>123</sup> Ungewezaje kuona aibu? Ungeweza kumkataa Mtu kama huyo, rafiki? Kumbuka.

<sup>124</sup> “Loo,” unasema, “Ndugu Branham, wahubiri wamehubiri kwa miaka mingi.” Ninajua, lakini moja ya siku hizi wataacha kuhubiri. Na jinsi mambo yanavyoonekana, inaweza kuwa ni sasa hivi. Utasikia mahubiri yako ya mwisho. Kusema kweli, huu unaweza ukawa wako wa mwisho.

<sup>125</sup> “Loo,” unasema, “Mimi ni mdogo.” Hiyo haijalishi. Kifo hakina upendeleo, wala umri wala uwezo.

<sup>126</sup> Je, utamkubali sasa kama Mwokozi binafsi, kwa kuinua mkono wako, ukisema, “Mungu, unirehemu”? Inua mikono yako pamoja na hawa wengine, na kusema, “Sasa nataka kumkubali Kristo.” Je, utainua mkono wako?

<sup>127</sup> Mtu aliyerudi nyuma, aseme, “Mungu, unirehemu. Ninataka kumrudia Kristo usiku huu, ili kesho iwe ndio ufufuo, mpya, kwangu.” Je, unaweza kuinua mikono yako? Inua mkono wako, useme, “Unirehemu. Nataka kuja sasa.” Je, utafanyi hivyo? Inua mkono wako, useme, “Nimekuwa mtu aliyerudi nyuma, lakini usiku wa leo...” Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki. Hilo ni jema. “Nitamkubali Kristo kama Mwokozi wangu binafsi. Nitamkubali usiku wa leo. Nimetangatanga, miaka mingi mbali na Mungu, lakini sasa narudi nyumbani.” Je, utamkubali usiku wa leo, ili kwamba huu upate kuwa ufufuo mpya kwako, maisha yako ya kale yaweze kumalizika?

<sup>128</sup> Mama huyu anakuja madhabahuni, kufanya maungamo yake, kusimama. Mtu mwingine anayetaka kupachukua mahali pao hapa, aje hapa pamoja naye, kwenye maungamo yao? Waweza kusimama, na kuja madhabahuni, pia? Madhabahu iko wazi. Hakika. Njoo moja kwa moja, sasa hivi. Ukitaka kusimama hapa na kuomba, itakuwa sawa tu. Njoo. Je, utakuja? Juu ya maungamo ya imani yako, juu ya kuamini kwako Mwana wa Mungu, utakuja sasa? Vema.

<sup>129</sup> Ni juu yako, kumbuka. Wewe ndiye. Je, wewe ni mwenye dhambi? Wewe umerudi nyuma? Wewe ni baridi na umemwacha Kristo? Nawe unataka kuinuliwa upya pamoja Naye sasa, uanze maisha upya? Nawe je, mume na mke ambao mmekuwa—mmekuwa nje kwa muda mrefu, mkgimbana nyumbani mwenu? Hivi hamtakuja na kunyoosha jambo hilo pamoja na Mungu na mmoja kwa mwingine sasa? Ifanyeni Pasaka iwe Pasaka halisi kwenu, mwanze makazi mapya.

<sup>130</sup> Vipi kuhusu wewe ambaye hujawahi kuwa, hujawahi kufanya maombi nyumbani kwako, unaenda tu nyumbani kutoka kanisani na kujaribu kuishi vyema uwezavyo, kamwe huikusanyi familia pamoja na kuomba? Ndio maana tuna uhalifu wa vijana na mambo tuliyo nayo. Hiyo ndiyo sababu nyumba za Marekani zimevunjika. Mbona usije, uanze upya usiku wa leo? Je, utafanyi hivyo? Umealikwa. Kumbukeni, mimi ni mhudumu wenu sasa; nitakuwa shahidi siku hiyo.

Wakati tumeinamisha vichwa vyetu, basi, sasa kwa maombi.

<sup>131</sup> Baba yetu wa Mbinguni uliyebarikiwa, usiku wa leo tunakuletea Wewe kusanyiko hili, katika kicho kitakatifu sana chenye uchaji tujuacho. Kwa unyenyekevu tunakikaribia Kiti Chako cha Enzi. Na baada ya huu Ujumbe usiku wa leo, huko, huko kuzikwa kukuu, Kamwe hakukaa kimya, nafsi Yake ilikwenda moja kwa moja katika yale maeneo na kuimaliza kazi ya Mungu, ambayo aliamriwa kuifanya. Basi kesho asubuhi, tutaona mahali alipopitia katika milki za juu, akishinda kila kitu, katika kufufuka Kwake. Lakini alifufuka asubuhi ya Pasaka kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu. Nasi tunaona ya kwamba Yeye alimtuma Roho Mtakatifu kurudi, kuwashtakia watu dhambi.

<sup>132</sup> Nasi tunaomba usiku wa leo, Bwana, ya kwamba wale walioinua mikono yao wapate kukumbukwa mbele Zako. Jalia uamuzi wao uwe kutoka moyoni mwao usiku wa leo, kwamba wamekupokea Wewe, na kukuamini Wewe, pia jalia watiwe muhuri kwa Muhuri wa ahadi usiku wa leo, Roho Mtakatifu. Tujalie, Baba. Kwa kuwa, tunawakabidhi Kwako, pamoja na Ujumbe huu usiku wa leo. Jalia Huo ubariki wale waliousikia, wale, Bwana, ambao wataenda nao nyumbani mwao, na kuuzamisha ndani kwa kilindi mioyoni mwao. Jalia waishi kwa Neno la Mungu. Tujalie, Baba, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Kristo. Amina.



*KUZIKWA* SWA57-0420  
(The Entombment)

MFULULIZO WA UAMSHO WA PASAKA

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumamosi jioni, tarehe 20 Aprili, 1957, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)